KIDATO CHA TATU

# MARUDIO YA TUMBO LISILOSHIBA

2. "... maendeleo yanadai mchango wa kila mtu, maskini na tajiri"
   a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
   b) Taja na ueleze sifa nne za msemaji katika dondoo hili. (alama 4)
   c) Mambo yepi mengine ambayo msemaji huhojiana na wenzake wanapokutana ? (alama 6)
   d) Taja na ueleze maudhui matatu yanayojitokeza katika dondoo hili. (alama 6)

3. Kwa kurejelea hadithi zozote tano katika diwani ya, 'Tumbo lisiloshiba na hadithi nyingine.' Jadili maudhui ya nafasi ya wazazi katika malezi. (alama 20)

**Eunice Kimaliro : Mtihani wa Maisha.**

4."…..ilmuradi mawazo yanamwadhibu sasa"
   a. Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
   b. Fafanua sifa za anayerejelewa katika dondoo hili. (alama 6)
   c. Onyesha mawazo yanayomwadhibu anayerejelewa na dondoo hili. (alama 10)

**Alfa Chokocho : Tulipokutana tena**

5. a. " Mamangu siku ile aliniamsha mapema."
   i) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
   ii) Tathmini umuhimu wa usimulizi wa mzungumzaji katika kuendeleza dhamira ya hadithi hii. (al 8)
   b. Onyesha jinsi mashaka linavyomwafiki mhusika mwenyewe katika hadithi ya "Ndoto ya Mashaka"(alama 8)

4.i) Sekta ya elimu ina changamoto nyingi.Thibitisha kwa kurejelea hadithi zifuatazo : (alama 20)
   i) Mapenzi ya Kifaurongo
   ii) Shogake dada ana Ndevu
   iii) Mwalimu Mstaafu
   iv) Mtihani wa maisha

5) '' Hakikubakia hata chakula kidogo cha sadaka ya mwenye njaa… ''
   i) Thibitisha ukweli wa kauli hii kwa hoja kumi ukirejelea hadithi ya Tumbo Lisiloshiba (al 10)
   ii) Jadili uhalisia wa hadithi ya Tumbo Lisiloshiba katika jamii ya leo kwa kutoa hoja kumi. (al 10)

4."Kesho kama sote tutaamka salama……….kama tutafungua milango ya nyumba zetu"….
   (a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)
   (b) Eleza tamathali mbili za lugha zilizotumiwa katika dondoo hili. (alama 4)
   (c) Eleza sifa sita za msemaji wa maneno haya. (alama 6)
   (d) Hadithi hii inaakisi mambo mengi yanayotendeka katika bara la Afrika. Taja mambo sita (alama 6)

5.Ukengeushi huzorotesha maendeleo ya kijamii. Jadili kauli hii ukirejelea hadithi ya 'Mkubwa'. (alama 20)

6. Kwa kuzingatia hadithi zozote tano katika diwani ya *Tumbo lisiloshiba na hadithi nyingine* eleza uozo wa jamii kama unavyojitokeza. (al 20)

7 "Kesho panapo majaaliwa. Kesho kama sote tutaamka…….. kama tutafungua milango ya nyumba zetu zinazosimamia juu ya ardhi hii adhimu…"
   a Eleza muktadha wa dondoo hili (al. 4)
   b Eleza sifa nne za msemaji (al. 4)
   c) Taja mbinu zozote mbili za lugha zinazojitokeza katika dondoo hili (al. 2)
   d Kwa kurejelea hadithi nzima onyesha namna jamii ya kisasa ina tumbo lisiloshiba (al. 10)

6. **"Rasta twambie bwana!"**
   a) Weka dondo katika muktadha (ala 4)
   b) Taja mbinu zilizotumiwa na mwandishi katika dondoo hili (ala 2)
   c) Ni kwa vipi mzungumziwa anamchukulia mwalimu mkuu kama hambe? (alama 4)

) Je, mtihani wa maisha ni amwani faafu ya hadithi hii. (alama10 )

adili mashaka ya Mashaka katika hadithi ya "Ndoto ya Mashaka" (alama 20)

:uku ukirejelea hadithi ya Tumbo Lisiloshiba na Shibe Inatumaliza, fafanua maudhui ya ukiukaji wa haki. (al.20)

"Penzi lenu na nani? . . . . Mgomba changaraweni haupandwi ukamea. Poteiea mbali mkate wee!"

a)Eleza muktadha wa dondoo hii. (alama 4)

b)Taja naufafanue mbinu mbili za lugha zilizotumiwa katika dondoo hili. (alama 4)

c)Onyesha vile maudhui ya utabaka yanavyo jitokeza katika hadithi nzima. (alama 6)

d)Eleza sifa sita za mzugumzaji kwenye dondoo. (alama 6)

likuwa kama vile katia saini ya kutiwa kitanzi bila ya kutambua vipengele vya sheria za utiaji huo wa kitanzi.

a)Fafanua tamathali mbili zilizotumika katika dondoo. (alama 4)

b)Jadili vipengele vitano vya sheria zinazorejelewa katika hadithi nzima. (alama 10)

c)Onyesha dhiki iliyompata mrejelewa kwa kukosa kivitambua vipengele hivyo. (alama 6)

"hebu sikiza jo! Pana hasara gani nzi kufia kidondani?

a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)
b) Tambua mbinu tatu za lugha zilizotumika katika dondoo hili na umuhimu wake (alama 6)
c) Onyesha jinsi dhana ya nzi kufia kidondani inabainika hadithini (alama 4)
d) Hali ya kutowajibika inajitokeza vipi katika hadithi? (alama 6)

Huku ukirejelea diwani ya Tumbo lisiloshiba fafanua matatizo yanayokumba vijana katika jamii (alama 20)

' ... alirejea tena na kumpasulia mbarika ... Ndugu usinifikirie mwendawazimu wala mlevi ..."

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
b) Eleza tamathali ya usemi uliyotumika. (alama 2)
c) "Ardhi ndicho kichocheo kikubwa cha unyama wa binadamu: Kwa kudondoa hoja kumi na nne, thibitisha ukweli wa kauli hii kwa kurejelea riwaya ya Kidagaa Kimemwozea. (alama 14)

'Ndoto ya uhuru barani Afrika imegeuka kuwa jinamizi, jinamizi inayowafanya wazalendo kulia"
Kwa kudokeza hoja ishirini, eleza jinamizi hili linalowafanya wazalendo kulia. (alama 20)

Eleza sifa za wahusika wafuatao. [alama 20]

) Mwalimu Musi
i) Jairo
ii) Sera
iv) Mke wa Jairo

" Acha nijiondelee duniani niwaachie wafanisi wafanikiwe."

Eleza muktadha wa dondoo hili . [alama 4]
Fafanua sifa za mhusika katika dondoo hili. [alama 8]
Fafanua mbinu zozote nne za kifani katika hadithi hii. [alama 8]

ogake Dada ana Ndevu – Alifa Chokocho .

apana cha ala, bwana. Liswmwalo lipo,kama halipo linakuja. Kumbuka msemo mabrafu wa siri ya kata iulize ungu . Mtungi wenyewe ni mimi ......"

Sura ya 5

# Kielelezo cha Maswali ya KCSE

1. "Tatizo kuu katika jamii ya Wahafidhina sio tu kuchaguliwa kwa kiongozi mwanamke." Fafanua kwa kurejelea riwaya hii.
2. "Upo wakati dau la mnyonge linapoenda joshi likashinda la mwenye nguvu."
   a) Eleza muktadha wa dondoo hili.
   b) Fafanua sifa **sita** za anayezungumza katika dondoo hili.
   c) Onyesha jinsi dau la mnyonge linavyoenda joshi kwa kurejelea wahusika wafuatao.
      i) Umulkheri
      ii) Kangata
      iii) Neema
   d) Kwa kujadili hoja **kumi** kutoka kwenye riwaya hii, onyesha kinyume katika kauli iliyopigwa mstari.
3. Mwandishi ametumia kinaya kwa ufanifu kuijenga riwaya hii. Fafanua.
4. "Ndivyo tunavyoishi ... Na usidhani ni kuishi huku ... ni kupapatika, kufufurishwa na matumbawe ya maisha ... pole ndugu, itabidi usahau mswala kwa hii mbacha."
   a) Eleza muktadha wa dondoo hili.
   b) Fafanua umuhimu wa anayeambiwa maneno haya katika kuijenga riwaya hii.
   c) Andika mifano **mitatu** ya sitiari katika dondoo hili.
   d) Kwa kurejelea hoja **kumi na nne**, onyesha jinsi raia wa Wahafidhina wanavyopapatika na kufufurishwa na matumbawe ya maisha.



5. "Ndugu, kunako matanga kumekufa mtu."
   a) Fafanua muktadha wa dondoo hili.
   b) Eleza sifa **nane** za msemaji katika dondoo hili.
   c) Jadili sitiari ya matanga kwa kurejelea riwaya hii.
6. Onyesha kwa kutoa mifano jinsi mbinu hizi zinavyotumika kuendeleza kuijenga riwaya hii.
   a) Usimulizi
   b) Mbinu rejeshi
   c) Mbinu elekezi
   d) Sadfa
   e) Dayalojia za wahusika
   f) Uzungumzi nafsia
7. "Vipi mtu utasahau ya kale na unaiishi hiyo kale?"
   a) Bainisha mbinu ya kimtindo iliyotumiwa katika kauli hii.
   b) Kwa kurejelea mifano **kumi**, eleza umuhimu wa mbinu hii katika kuijenga riwaya hii.
   c) Bainisha nafsi ya usimulizi katika kauli hii.
8. "Kwa nini nishuku kunyang'anywa kwa urithi na hali ni tendo la kikaida humu?"
   a) Fafanua muktadha wa dondoo hili.
   b) Eleza umuhimu wa mbinu ya kimtindo iliyotumiwa katika dondoo hili.
   c) Andika sifa ya jamii ya Wahafidhina inayodokezwa na kauli hii.
   d) Kwa kurejelea mifano **kumi na mitano**, onyesha jinsi sifa hii inavyoendelezwa katika riwaya hii.
9. Onyesha nafasi ya matumizi mabaya ya vileo katika kuizorotesha jamii ya Wahafidhina.
10. "Nitatokomea kokote kule. Afadhali kuishi Jahanamu kuliko husuni hii yako."
    a) Fafanua muktadha wa dondoo hili.
    b) Eleza sifa za anayeelekezewa kauli hii.

11 - 20

c) Onyesha Jahanamu aliyoiishi msemaji na wengine wa jinsia yake katika riwaya hii.

d) Jadili Jahanamu za aina nyingine katika riwaya.

11. Jadili umuhimu wa wahusika wafuatao katika kuijenga riwaya hii.

   a) Sauna
   b) Shamsi
   c) Apondi
   d) Kimondo

12. Onyesha jinsi uozo wa maadili unavyohatarisha maisha ya binadamu katika riwaya.

13. "Hata anapowaelekezea macho sasa hivi hawaoni. Anachoona ni malaika wa heri waliotumwa kutoka mbinguni ..." = 172

   a) Fafanua muktadha wa dondoo hili.
   b) Eleza umuhimu wa msemaji katika kuijenga riwaya hii.
   c) Kwa kurejelea riwaya hii, onyesha heri wanayoipata vijana.

14. Jadili namna masuala yafuatayo yalivyoshughulikiwa katika riwaya.

   a) Utabaka
   b) Unyanyasaji wa kijinsia
   c) Ukoloni mamboleo

15. "Usiisifu njaa ya mbwa kabla usiku haujaingia ukahakikisha kuwa mbwa amelala njaa." 183

   a) Eleza muktadha wa dondoo hili.
   b) Eleza umuhimu wa mzungumzaji asilia wa kauli hii katika kuijenga riwaya hii.

16. Tathmini umuhimu wa mbinu zifuatazo katika kuijenga riwaya ya *Chozi la Heri*

   a) Nyimbo
   b) Barua



17. "Moyo wangu, uchungu na kukata tamaa kulikonikumbatia nilipotoka hospitali hakuwezi kumithilika." 155

   a) Eleza muktadha wa dondoo hili.
   b) Bainisha aina mbili za taswira katika dondoo hili.
   c) Andika tamathali nyingine tatu za usemi zinazojitokeza katika dondoo hili.
   d) Bainisha toni ya kauli hii.

18. Riwaya ya *Chozi la Heri* inakatisha tamaa. Thibitisha kwa hoja **ishirini**.

19. Jadili mchango wa mwanamke katika kuivunja jamii ya Wahafidhina.

20. 'Mwandishi amemtetea mwanamume.' Thibitisha.

21. 'Dhamira kuu ya *Chozi la Heri* ni kuhimiza mshikamano wa kijamii.' Fafanua kwa kurejelea hoja **kumi**.

22. Jadili nafasi ya utamaduni katika kuyajenga na kuyabomoa maisha.

23. 'Wasomi wa Wahafidhina wamekengeuka.' Fafanua.

24. "Sasa umerejea kwenu kupata tumekuporomosha kwa viganja vyetu wenyewe."

   a) Eleza muktadha wa dondoo hili.
   b) Fafanua sifa za mzungumzaji.
   c) Jadili namna wanyonge walivyokuporomosha kwao wenyewe.